Geita Leo

Halmashauri ya Mji Geita
GEITA TOWN COUNCIL

Toleo Na. 2 Tarehe 01/01/2018 hadi 31/03/2018

MRADI WA UJENZI WA JENGO LA UTAWALA

Pichani ni muonekano wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Mji Geita baada ya kukamilika.Mradi wa ujenzi wa jengo hilo unatekelezwa na mkandarasi MS MAGACON Company Limited ya Dodoma. Mradi huu utagharimu kiasi cha Shilingi 2,647,693,572 kwa awamu ya kwanza, kutoka Serikali kuu na mapato ya ndani ya Halmashauri.

UJENZI WA ZAHANATI YA NYANGUKU AMBAO UMEKAMILIKA NA KUFUNGULIWA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA KWA WANANCHI WAPATAO 12,199 WAKAZI WA VIJIJI VITATU NA MITAA MIWILI YA KATA HIYO. UJENZI WA ZAHANATI YA NYANGUKU UMEGHARIMU KIASI CHA SHILINGI MILIONI 168,742,000 KUTOKA SERIKALI KUU, HALMASHAURI YA MJI GEITA NA MCHANGO WA WANANCHI WA KATA YA NYANGUKU. WANANCHI WAMEISHUKURU SERIKALI KWA KUTHAMINI AFYA ZAO NA KUWASOGEZEA KARIBU HUDUMA AMBAYO AWALI WALIKUWA WAKIIPATA BAADA YA KUTEMBEA UMBALI MREFU.

Ujenzi wa Shule ya Sekondari Nyabubele katika kata ya Kasamwa ukiwa unaendelea. Kukamilika kwa vyumba sita vya madarasa na Ofisi moja ya walimu kutawezesha wanafunzi kutoka katika kijiji hicho kupata elimu karibu na majumbani kwao tofauti na karaha wanayoipata hivi sasa kwa kutembea umbali mrefu kwenda shule. Pia ukamilifu wa Shule hii kutapunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari Kasamwa. Ujenzi wa Shule ya Sekondari Nyabubele hadi kukamilika kwake inakadiriwa kutumia kiasi cha Shilingi 350,000,000 (Shilingi Milioni mia tatu hamsini) kutoka Serikali kuu, Halmashauri ya Mji na mchango wa wananchi.

Bwalo la chakula kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Kasamwa

Bweni la Wasichana wa kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Kasamwa

Madarasa mawili ya Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Kasamwa.

UJENZI WA MIUNDO MBINU YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO NA SITA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KASAMWA. MAJENGO YA MADARASA MAWILI, BWALO KWA AJILI YA HUDUMA YA CHAKULA NA BWENI KWA AJILI YA WASICHANA 60 YAMEKAMILIKA. KUKAMILILIKA KWA MAJENGO HAYO KUTAIWEZESHA SHULE YA SEKONDARI KASAMWA KUPOKEA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO MWEZI WA SABA MWAKA 2018. NA KUFANYA HALMASHAURI YA MJI GEITA KUWA NA IDADI YA SHULE NNE ZA UMMA AMBAZO ZINADAHILI WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO. UJENZI WA MIUNDO MBINU YA KIDATO CHA TANO NA SITA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KASAMWA UMEGAHRIMU KIASI CHA SHILINGI 410,000,000/=(SHILINGI MILIONI MIA NNE NA KUMI) .

Mpendwa msomaji wa Jarida letu tunakukaribisha kutembelea ukurasa wa Tovuti ya Halmashauri ya Mji wa Geita kupitia anwani ya www.geitatc.go.tz ili kupata habari za matukio muhimu yanayoendelea katika mji wetu, Miradi inayotekelezwa na masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Pia unaweza kuwasilisha maoni na malalamiko kupitia Tovuti hiyo.

MATUKIO KATIKA PICHA

Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Mhandisi Robert Gabriel akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa Zahanati ya Nyanguku katika kata ya Nyanguku Halmashauri ya Mji Geita.

Wanafunzi kutoka Halmashauri ya Mji walioshiriki mashindano ya Olimpiki Maalum mjini Zanzibar wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Mkoa na Halmashauri ya Mji Geita baada ya kurejea na ushindi .

Madiwani wa Halmashauri ya Mji Geita wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Geita(hayupo pichani) wakati wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya pili hivi karibuni.

Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhandisi Robert Gabriel akishiriki kuchimba msingi wa Zahanati ya Nyamalembo ambayo inajengwa kwa nguvu za wananchi.

UJENZI WA BARABARA YA KATUNDU—AMERICAN CHIPS 1.2 KM, MITI MIREFU 1 0.2KM NA MITI MIREFU 2, 0.7 KM KWA KIWANGO CHA LAMI UTAGHARIMU KIASI CHA SHILINGI BILIONI 1.4 KUTOKA KATIKA MRADI WA ULGSP CHINI YA BENKI YA DUNIA.

Ujenzi wa vizimba kwenye Soko kuu Geita Mjini.

PICHA IKIONYESHA MUONEKANO WA SOKO KUU GEITA MJINI BAADA YA UJENZI WAKE KUKAMILIKA.

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI GEITA KWA NIABA YA WATUMISHI WOTE WA HALMASHAURI YA MJI GEITA, ANAWATAKIA WANANCHI WOTE KATIKA HALMASHAURI YA MJI GEITA HERI NA BARAKA YA MWAKA MPYA 2018.

TUUNGANE PAMOJA KATIKA KAZI ILI KULETA MAENDELEO YA MJI WETU.

Jarida hili hutolewa bure kila baada ya Miezi mitatu na Kitengo cha TEHAMA, Halmashauri ya Mji Geita,

S.LP 384 Geita, Simu Na. 0282520437, Nukushi Na. 0282520437, Barua pepe: td@geitatc.go.tz, Tovuti: www.geitatc.go.tz